# Muakiso wa Uhalisi wa Kauli za Mhusika Mlevi katika Fasihi ya Kiswahili

**Lazaro Mlelwa**
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
*lmlelwa@yahoo.com*

**Gerephace Mwangosi**
Chuo Kikuu Katoliki Ruaha

***Ikisiri***
*Tamthiliya ya Kiswahili ni miongoni mwa kazi za kisanaa zenye wajibu mkubwa wa kuijenga jamii katika hali mbalimbali kupitia wahusika wake. Kwa kawaida, wahusika hudhibitiwa na kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na muktadha wa utunzi, hasa mawazo yanayowahusu waandishi kulingana na falsafa zao, mazingira yao, utamaduni wao, hali ya maisha na harakati zilizopo katika jamii inayohusika. Makala haya yanachunguza muakiso wa uhalisi wa kauli za mhusika mlevi katika kazi za kifasihi. Zaidi pia, kuna urejeleaji watamthiliya teule za Lina Ubani (1984) na Mabepari wa Bongo (2007). Data za msingi za makala haya zimepatikana maktabani kwa kudurusu tamthiliya teule zilizobainishwa. Mapitio ya nyaraka zilizotumika kuthibitisha data za msingi pia zimepatikana kwa mbinu za usomaji wa nyaraka. Uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa umeongozwa na nadharia ya Ucheshi. Makala haya yanahitimisha kuwa mhusika mlevi ni mojawapo ya mawakala wa kazi za kifasihi kwa kuwa huyafichua na kuyaweka wazi mambo yote yanayoshindikana kusemwa na wahusika wakiwa katika ung'amuzi tambuzi.*

**Maneno Muhimu**: Muakiso, Mlevi, Mhusika, Ucheshi, Tamthiliya ya Kiswahili

## 1.0 Utangulizi

Ushahidi wa zamani zaidi kuhusu kutumika kwa mhusika mlevi katika utanzu wa tamthiliya unapatikana katika jamii ya Wayunani waliomtumia katika mashindano ya sanaa za maonesho ya Kiramsa tangu karne ya 5 Kabla ya Kristo (KK) huko Athene. Bakola (2006) anawataja na kuwaelezea Cratinus na Aristophanes kuwa ni baadhi ya wanasanaa waliomtumia mhusika mlevi katika kazi zao za fasihi ili kuonesha na kuongeza sanaa na ubunifu wao katika sanaa za maonesho na mashindano ya ushairi yaliyokuwa yakifanyika huko Uyunani. Shakespeare (1579) alimtumia mhusika mlevi katika mchezo wake wa kuigiza ulioitwa *The Taming of the Shrew*. Mchezo huo uliandikwa mwaka 1623, baada ya kifo chake, na kuchapwa mwaka 1990. Kwa kawaida, waandishi huchochewa na yale yanayotokea katika jamii zao; hivyo basi, wahusika hawana budi kuakisi yaliyomo katika jamii zao. Tamthiliya ya Shakespeare imemsaidia mtafiti kumchunguza mhusika mlevi alivyotumika kulingana na wakati na muktadha wa uandishi wake. Makala haya yamezingatia kuwa muktadha wa uandishi wa tamthiliya za *Lina Ubani* na *Mabepari wa Bongo* ni tofauti kabisa na nyakati za uandishi wa Shakespare. Mwachano wa kiwakati umezingatiwa katika uchunguzi wa makala haya.

Moliere, msanii wa Kifaransa, aliandika tamthiliya ya *The Doctor Inspite of Himself* (1911),kitabu ambacho kimejengwa kwa kiasi kikubwa na mbinu ya matumizi ya mhusika mlevi kama wenzo wa kisanaa wa kufikisha ujumbe kwa jamii iliyolengwa na mwandishi. Kwa ujumla, kazi ya Shakespeare na ile ya Moliere zimesaidia kujenga uelewa wa kutosha kuhusu nafasi na majukumu ya mhusika mlevi katika kazi za kisanaa; na jinsi waandishi wanavyomtumia katika kazi zao.

Kadiri jamii za ulimwengu zilivyozidi kukua na kuendelea ndivyo kazi mbalimbali za kifasihi zilivyobadilika zikiakisi mabadiliko hayo. Matumizi ya wahusika walevi lilikuwa ni jambo lililotokea mara kwa mara katika tanzu mbalimbali za fasihi.Tamthiliya zilizotumia wahusika walevi zilizidi kuenea mpaka kufikia miaka ya 1850. Waandishi wa Marekani waliweza kuigiza tamthiliya mbalimbali katika nchi yao zikiwa na mhusika mlevi. Baadhi yake ni tamthiliya ya *The Drunkard* ya Smith katika gazeti la *American Temperance* la Desemba, 1851. O'Cannor aliandika hadithi fupi iliyoitwa *The Drunkard* (1948) iliyozungumzia watoto, ulevi, pombe, udhalilishaji na hekaya iliyoakisi hali halisi ya maisha katika jamii yao katika kipindi hicho. Kutokana na maendeleo ya tamthiliya na matumizi ya mhusika mlevi kuongezeka, maswali yanayoibuka ni haya: je, wahusika hawa wana nini cha ziada wanapolinganishwa na wahusika wengine? Kwa nini uhusika wao unapendelewa na waandishi? Maswali haya ni ya msingi katika kujenga uelewa kuhusu wajibu wa mhusika mlevi katika vitabu teule vilizochunguzwa.

Mwandishi wa tamthiliya iliyoitwa *Uncle Tom's Cabin* (1853) amemtumia mhusika mlevi pia. Tofauti kidogo na tamthiliya zilizotangulia, tamthiliya hii ilikuwa inapinga ulevi na utumwa. Aidha, tamthiliya ya *Uncle Tom's Cabin* ilitumika kuonesha udhaifu wa mhusika mlevi katika kazi za kisanaa. Kazi nyingine zilizofuata zilizowatumia wahusika walevi ni pamoja na *Ten Night in Bar Room* iliyoandikwa na Arthurs (1858) na Wilder aliandika *Our Town* (1930). Kazi za waandishi hawa, kwa ujumla wake, zimesaidia kujua jinsi mhusika alivyochukuliwa na jamii alimoishi, alivyoonekana na alivyohesabiwa katika mwenendo wake mzima. Hali hii

huwafanya baadhi ya wanajamii kumtazama mhusika mlevi kama mwendawazimu ama kituko kulingana na namna anavyotumiwa katika kazi za kisanaa.Mbali na waandishi hawa wa Kimagharibi, matumizi ya mhusika mlevi katika fasihi yalijitokeza kwa waandishi wa Afrika. Kazi nyingi za mwanzo katika fasihi andishi ya Kiafrika zilijichomoza kutoka katika fasihi simulizi. Riwaya ya Amos Tutulola ya *The Palm-Wime Drinkard* (1952) alimtumia mhusika mlevi kuchota uhusika wake kutoka katika ngano za jamii ya Kiyoruba. Kule Afrika ya Kusini, Jordan (1973) akiifafanua fasihi ya Kiafrika, hasa jamii ya Wa-Xhosa wa Afrika ya Kusini, alimtumia mhusika mlevi akilinganisha maisha ya Wakristo na wasio Wakristo. Nchini Tanzania, Kezilahabi katika *Rosa Mistika* (1975) anamtumia mhusika mlevi kusawiri hali ya maisha katika jamii za kifukara. Nyoni (*Mabepari wa Bongo*) na Muhando (*Lina Ubani*) wanaingia katika kundi la waandishi wa Kiafrika waliomtumia mhusika mlevi kulingana na miktadha ya uandishi wao.

Tamthiliya zilizolengwa zimetumika kwa kuwa zinaakisi uhalisi wa jamii katika kipindi cha baada ya uhuru na kifo cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Baba wa Taifa, aliyeasisi misingi ya Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea nchini Tanzania. Muhando amebainisha changamoto za kijamii na kisiasa baada ya Watanzania kupata uhuru, hasa miaka ya sabini, kipindi kilichotamalaki utekelezaji wa Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea nchini Tanzania. Kwa upande mwingine, Nyoni ameangazia hali za kisiasa na kiuchumi kipindi cha takribani miaka 10 baada ya kifo cha Mwalimu J. K. Nyerere. Makala haya yameziteua tamthiliya za *Mabepari wa Bongo* (2007) na ile ya *Lina Ubani* (1984) ili kuchunguza uhalisi wa kauli za mhusika mlevi katika fasihi ya Kiswahili.

## 1.1 Mbinu na Upeo wa Mada

Tamthiliya ya Kiswahili katika jamii za Afrika Mashariki hujengwa katika misingi ya muktadha wa utunzi unaodhihirisha wazi mfungamano mahsusi uliopo baina ya wakati na mahitaji ya jamii. Hali hii huwafanya watafiti na wahakiki wengi (Matteru, 1982; Mlacha, 1985; Senkoro, 2006; Mlelwa, 2012; Mnigo, 2015; Shemweta, 2015) kuzishughulikia kazi zake kwa misukumo na mitazamo mbalimbali. Kipengele cha uhalisi wa kauli za mhusika mlevi, hasa jinsi anavyokua na kubadilika kifikra na kiwakati hakijachunguzwa kwa undani wake. Makala haya yamechunguza muakiso wa uhalisi wa kauli za mhusika mlevi kwa kurejelea vitabu teule. Data za msingi zimepatikana katika tamthiliya teule za *Lina Ubani* (1984) na *Mabepari wa Bongo* (2007). Tamthiliya hizo zimeteuliwa kwa kuwa zina mawanda ya kutosha yaliyotuwezesha kupata data zilizolengwa katika makala haya. Mapitio ya nyaraka zilizotumika kuthibitisha na kujaziliza data za msingi pia zimepatikana kwa mbinu za usomaji wa nyaraka. Uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa umeongozwa na nadharia ya Ucheshi.

## 1.2 Mkabala waUhakiki

Nadharia ya Ucheshi imekuwepo tangu enzi za Plato miaka ya 429 na 423 KK. Nadharia hii iliendelezwa na wanasaikolojia mashuhuri waliokuwa wamebobea kwenye utafiti kuhusu vyanzo vya ucheshi, vichekesho na vicheko. Walichunguza ni kwa nini mwanadamu ndiye mnyama pekee anayeweza kucheka; na ni kwa nini anacheka. Kicheko huja baada ya ucheshi na kinyume chake (Potter, 1954; William & wenzake, 1976). Godkewitsch (1976) anaeleza sababu tatu zinazosababisha hisia ambazo ni: mtu kuwa katika kiwango cha juu cha hisia kali, majumuisho kamili ya hisia-indushi na hisia-

nasibu za hali ya kichochezi. Ucheshi unasababishwa na masuala ya kibaolojia, matumizi ya mbinu za kifasihi na zisizo za kifasihi (Senkoro, 2004; Wamitila, 2008). Majawapo ya majukumu ya ucheshi ni kupata makadirio yanayoonekana; na una athari kubwa katika kupunguza migogoro ndani ya jamii, kuweka wazi upinzani uliopo na kutoa maagizo.

Nadharia ya Ucheshi katika makala haya imetumika kuyatazama mazingira ya asili ya jamii kuwa ndiyo huamua namna kazi ya kifasihi inavyotakiwa kuwa. Mawazo ya waandishi yamechunguzwa kupitia mhusika mlevi anayewasilisha mambo bila aibu, uoga na kuhofia jambo lolote linaloweza kumsibu. Hali hii huitazama fasihi kama kitengo kilicho na uwezo wa kuakisi mifumo inayodhibitiwa na miundo ya kijamii (Chapman, 1976). Mtafiti alimchunguza mhusika mlevi kuwa ni malighafi ya fasihi. Wandishi wa vitabu teule waliwekwa katika muktadha wao wa kawaida na halisi ili kujua mwenendo na shughuli za mhusika mlevi kwa kuwa ulevi wao ndio kiungo chao.Mhusika mlevi alitazamwa kwa undani jinsi alivyoakisi na kuyachunguza masuala ya kijamii na kuyaweka kama yalivyo, yanavyoaminika na kukubalika kupitia tamthiliya zilizolengwa. Pia, nadhari ya Ucheshi imetumika kuchunguza uhusiano uliopo baina ya fasihi na jamii kupitia kwa mhusika mlevi katika vitabu teule.

## 1.3 Muakiso wa Uhalisi wa Kauli za Mhusika Mlevi

Kwa kawaida, mhusika mlevi anapolewa, hasa akiwa chakari, huanza kuongea masuala mbalimbali yaliyoko mioyoni mwao. Uhusiano wa pombe na ufanyaji kazi wa ubongo husababisha mlevi kunena yale yaliyoko moyoni mwake bila simile, yakiwamo yanayomsibu, yanayomkera na kuiandama jamii

yake (Arthurs, 1858). Hii inaonesha wazi kwamba, kuna uhalisi fulani katika maneno ya mlevi. Pia, inaonesha kuwapo kwa mambo kadha wa kadha yanayohusu maisha na harakati za maendeleo ya jamii inayohusika. Huu ndio msingi wa makala haya kuchunguza muakiso wa uhalisi wa kauli za mhusika mlevi kwa kurejelea vitabu teule kama ilivyofafanuliwa katika sehemu inayofuata.

### 1.3.1 Muakiso wa ukweli kuhusu siasa

Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ilijitokeza nchini Tanzania mara baada ya kuasisiwa kwa Azimio la Arusha. Watu wote walihimizwa kuishi katika vijiji vya ujamaa wafanye kazi kijamaa katika hali ya umoja na ushirikiano (Nyerere, 1968). Waandishi na watunzi wengi waliandika kuhusu ujenzi wa jamii mpya ya kijamaa iliyofuata misingi ya haki na usawa wa binadamu. Hata hivyo, siasa ya ujamaa haikupata nafasi ya kukua na kukomaa kwa kuwa ilikosa mashiko kwa wananchi walio wengi. Maneno ya Mwanahego katika *Lina Ubani* yanaakisi ukweli wa kushindwa kwa siasa ya Ujamaa na Kijitegemea. Mwandishi anaeleza:

> *Umoja na mke wako mnayejifunika wote shuka moja. Mwanahego na wewe tutakutana wapi ndipo tuwe na umoja… Shwaini… wewe juu ya kilima, mimi bondeni…. Unakunywa wiski, Mwanahego chibuku… Umoja…. Akaa! Mie sina umoja* (Mlama, 1984: 23).

Mwanahego anakejeli harakatiza Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea iliyowahimiza watu wote kuishi kwa umoja na ushirikiana, hasa wakiwa katika vijiji vyao. Lengo mojawapo la serikali kuwaweka wananchi pamoja lilihusu kuinua maisha ya

wananchi wake kwa kuwasogezea huduma muhimu za kijamii zikiwamo: afya, elimu, maji, na barabara. Jitihada zilikumbwa na mwitikio hasi kutoka kwa wananchi kama ilivyodokezwa na Mwanahego hapo juu. Jambo hilo ndilo linalooonesha kuwa mlevi anapoongea yapaswa asikilizwe na sio kupuuzwa. Katika shairi la '*Azimio*', Kezilahabi anaonesha jinsi siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ilivyoshindwa kukua na kukomaa kutokana na sababu mbalimbali zilizokuwepo wakati huo. Kezilahabi (2008:18) anaeleza:

*Azimio sasa ni mabaki ya chakula,*
*Kwenye sharubu za bepari,*
*Kalamu inayovuja,*
*Katika mfuko wa mwanafunzi,*
*Vumbi zito,*
*Baada ya ng'ombe kupita,*
*Hakunyolewa,*
*Hakupewa kalamu mpya,*
*Na njia haikuzibwa,*
*Kilichosalia sasa,*
*Ni punje za ulezi,*
*Zilizosambazwa jangwani,*
*Na mpandaji kipofu.*

Kezilahabi anaiona siasa ya Ujamaa na Kujitegemea kama mabaki ya chakula kwenye sharubu za bepari. Hali hii ina maana kuwa siasa za ujamaa zimevamiwa na watu wenye uchu wa mali na pesa. Kulingana na Kezilahabi, hii ina maana kuwa mfumo wa Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea umechuja na kudhoofika kabisa kutokana na usaliti uliofanywa na baadhi ya viongozi waliokuwa wameshika hatamu. Katika *Mabepari wa Bongo*, mwandishi anamchora mheshimiwa Guduza kama kiongozi anayehujumu mali za wananchi kutokana na uchu wa

kujilimbikizia mali. Hali hii inaendelea kuimarika na kutazamwa kama tishio kwa vizazi vya Afrika ya sasa na baadaye. Bibi anasema:

> *Ewe mjukuu wangu uliyelaaniwa,*
> *Kaa kitako huko kuzimu unisikilize.*
> *Hayo uliyofanya kabla hujafa,*
> *Ndiyo aliyokufundisha mwalimu?*
> *Ndiyo aliyokuachia mwalimu?*
> *Ndiyo aliyokurithisha mwalimu?* (Nyoni, 2007:15).

Hadithi inayotambwa na bibi, inadhihirisha namna Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ilivyodhoofishwa na viongozi wenye tamaa ya kujilimbikizia mali. Baada ya siasa ya ujamaa kushindwa na kufifia kabisa, siasa za kibepari ziliinuka na kushika hatamu na zikawafanya watu wengi kujiingiza katika tamaa za kupora na kujilimbikizia mali za umma kwa maslahi binafsi (Mayega, 2006). Tamaa hizo ndizo zilizozaa dhana ya ufisadi na uhujumu uchumi zilizogeuka kuwa janga la kitaifa na mataifa mengi hapa Afrika. Kauli za mlevi hazipaswi kupuuzwa bali kutendewa kazi pale inapobidi (Dickens, 1954). Licha ya kuwa mlevi huongea baadhi ya mambo akiwa amelewa, lakini anachokiongea akiwa katika hali hiyo, ndicho kinachoakisi ukweli halisi wa kile kilichomo katika jamii ambamo kazi inayohusika imeandikiwa.

### 1.3.2 Muakiso wa ukweli kuhusu uchumi

Uchumi ni mojawapo ya nyanja muhimu katika maisha ya jamii na taifa lolote. Uchumi una nafasi kubwa katika mchakato na mfumo mzima wa maisha na maendeleo ya taifa na watu wake. Bila kujenga uchumi imara na endelevu, maendeleo ya taifa

hayawezi kuwa chombo cha kuwasaidia wananchi na ustawi wa taifa lao. Jitihada za kujenga uchumi imara na endelevu ziliwekwa katika misingi ya Siasa ya Ujamaa na Kujitegemeabaada ya kupatikana uhuru nchini (Nyerere, 1974). Katika kipindi hicho, watu walitakiwa kuishi kijamaa licha ya hali mbaya kiuchumi iliyokuwa imetamalaki katika kipindi hicho. Bidhaa muhimu ziliadimika nchini. Watu walinunua vitu kwa foleni na wakati mwingine hawakupata walivyovihitaji. Hali hiyo inadhihirishwa na Mwanahego anaposema, lakini mke wangu anajua umoja. Alivyoona sina hela za kulisha watoto, kachukua watoto wote kwa mama yake! Siyo wewe una kitambi unasema una umoja na Mwanahego. Aka! Unitue! (Nyoni, 2007: 46).

Mwanahego anaonesha jinsi uchumi wa nchi ulivyoyumba na kuporomoka katika kipindi hicho cha ujenzi wa Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Hakuna aliyeweza kusema hayo na kuyaweka wazi ili kukwepa mkono wa chuma wa dola. Mwanahego ameweza kuyasema bila wasiwasi, lakini yasingeweza kuelezwa na mtu mwenye akili timamu kwa kuhofu nguvu na udhibiti wa kimamlaka. Mwanahego aliweza kuyasema hayo akiwa katika hali ya ulevi. Pombe ndizo zilizomwondolea aibu, hofu na woga na kumpeleka katika ulimwengu wake unaompa ujasiri kwa kuwa huwa katika hali ya nusu urazini. Akiwa katika hali hiyo, pia aliweza kusema yaliyokuwa katika jamii yake.[16] Jamii pia ilikiri kuwa Mwanahego anasema ukweli. Mwandishi anaeleza:

> ‘Mlevi’ ‘siyo’ ‘mlevi’
> ‘Mlevi’ si ‘mlevi’
> ‘Maneno yake ya kweli’ (uk. 49).

[16] Taz. *Lina Ubani* (uk. 38) Sara anasema, “Nitakaa hapa mpaka mtakaponipa chakula. Msiponipa leo, kesho nitakaa, na kesho kutwa. Nikiondoka bure, nitaondoka na mtu.

Nukuu hii inaonesha jinsi jamii inavyokiri kuwa maneno ya mlevi yanaakisi ukweli. Kigezo muhimu katika uwasilishaji wa maisha katika kazi za kihalisia ni dhana ya ushabihikweli (Selden, 2005). Msisitizo wa kazi hizo ni kujaribu kufikia ukweli uliopo katika jamii inayohusika. Mawazo ya Mwanahego yanawekwa wazi kwa njia ya nusu urazini na yanaleta ucheshi kwa watazamaji. Ucheshi unajengwa na kejeli anayoionesha kuwa viongozi wana uwezo mkubwa wa kiuchumi, lakini wananchi wanaishi katika hali ya umaskini kiasi cha kushindwa hata kulea watoto wao. Ucheshi hutegemea sana kutokuwepo kwa ukubalifu kati ya hali ya viongozi na wananchi wao kiuchumi.

Katika tamthiliya ya *Mabepari wa Bongo*, mwandishi amemtumia MC Kilevi kumulika ukweli uliopo kuhusu suala la uchumi katika jamii. Uchumi wa leo unaonekana kutekwa na kuwekwa mikononi mwa wawekezaji kutoka nje; na si mikononi mwa wazawa kama ilivyo katika mataifa mengi barani Afrika (Shivji, 2002). Kiuhalisi, wahusika wengine wasingeweza kuuliza swali alilouliza MC Kilevi kwa kuwa limejengwa katika hali ya uchokozi unaoichokoza serikali. Maneno, muonekano na ucheshi alionao unachagizwa na kilevi alichotumia kinachomweka katika hali ya nusu urazini. MC Kilevi anaeleza kuwa hii kali! Wawekezaji wote wanatoka Usauzi? Hakuna wanaotoka nchi nyingine? Halafu wote Wazungu… (Nyoni, 2007: 19).

Kauli ya MC Kilevi inaakisi hali halisi ya maisha ya Mtanzania kiuchumi, hasa katika kipindi hiki kilichotamalaki Será za Utandawazi na Mfumo wa Soko Huria. Wawekezaji ndio walioshika uchumi wa nchi kupitia kwa viongozi wenye uchu

wa mali na rasilimali za umma. Uhalisi wa maisha ya Kitanzania, licha ya ule wa kisanaa, unaonesha namna wananchi walivyoangukia katika hali ngumu ya maisha kwa kuwa bado viongozi wao, walio wengi, wana tamaa ya kupenda pesa zaidi kwa kupuuza utu wa binadamu na misingi ya uongozi na utawala bora wa haki na demokrasia (Mbonde, 2002). Kazi ya sanaa ni kumulika ili kuyaweka wazi yale yote yanayoathiri ustawi wa maendeleo ya taifa. Madhumuni ya waandishi yanalenga kuijenga na kuichochea jamii ili iweze kuyatafakari na kuyachukulia hatua za kuyaendeleza yenye tija na kuyaondoa yasiyofaa kwa maslahi mapana ya umma.

### 1.3.3 Muakiso wa ukweli kuhusu jamii

Muakiso wa kauli za mlevi, kijamii hujengwa na mambo halisi yaliyopo katika jamii. Yapo mambo yanayofumbiwa macho na wahusika wengine, lakini mlevi huyasema bila kujali athari zinazoweza kutokea kwake. Aghalabu, mlevi huropoka kuutambulisha uhalisi wa maisha ya jamii yake bila kujali anasema wapi na kwa nani. Hali hiyo ni kwa sababu sanaa ya kunakili kutoka katika asili ipo katika hatua za maisha ya kila siku na inawakilishwa kwa msomaji badala ya kuoneshwa katika picha za ulimwengu wa kufikirika (Faulkner, 1977). Usahihi wa uwasilishaji ni ule wa uhalisi unaomzunguka kila siku. Mathalani, katika tamthiliya ya *Lina Ubani* mwandishi kwa kumtumia mhusika mlevi anaangaza ukweli wa maisha ya jamii kwa njia ya kindoto uliyo katika akili yake baada ya kulewa. Anasema:

> *Maneno hayo kamwambie hawara yako anayepanda gari kila anapokwenda… Wakataka kunigonga… Shwaini… "Huyu*

> *mlevi." Mlevi baba yako huyo unayetembea naye... Mafuta wanaendeshea magari ya kulalia watoto wetu*…. (Nyoni, 2007: 47).

Nukuu hii inaonesha maneno ya mlevi yanavyoakisi ukweli uliopo katika jamii ambapo wanaume, hasa watu wazima wenye mchezo wa kufanya mapenzi na mabinti wadogo. Kwa namna fulani, ni namna ya kumdhalilisha mtu kwa kumwambia 'Mlevi baba yako unayetembea naye'. Maneno hayo yana maana kwamba, baba anafanya mapenzi na mtoto wake wa kike. Maneno hayo yanaibua ucheshi na vicheko kwa wasomaji na wasikilizaji. Vilevile, huonesha namna wanaovyotumia pesa za umma kwa umalaya kutokana na kusheheni kwa vimada. Mali za umma zilitumika ovyo katika starehe binafsi na shughuli binafsi bila kujali wanavyoliingizia taifa hasara kubwa bila sababu za msingi. Hali hiyo imewafanya wanaume kujitengenezea mamlaka na utamaduni wa kuwasaidia katika maslahi yao ya kuwatawala wanawake (Legulegu, 2016). Halikadhalika, ukahaba umewafanya wanawake kuwa kama bidhaa. Hiki ndicho kinachomfanya Mwanahego kusema kwa hasira kwa kuwa pesa za umma hazitumika kwa maslahi ya umma.

### 1.3.4 Muakiso wa ukweli kuhusu uongozi

Katika historia ya maendeleo ya jamii, uongozi ulianza tangu kale pale wanadamu wa kwanza walipoanza kuzaliana na kuongezeka zaidi (Davidson, 1970). Mwanaume akawa kiongozi wa familia yake. Kadiri jamii ilivyoongezeka, suala la uongozi kifamilia lilipanuka zaidi na watu wakawa na watawala waliohusisha familia kadhaa. Maendeleo katika jamii yalipozidi, uongozi ukawa dhana pana sana ambayo ilichukua sehemu kubwa ya jamiilugha. Matokeo yake, matabaka katika

jamii yalijitokeza kwa uwazi zaidi. Katika kazi za fasihi, uongozi aghalabu husawiriwa kwa namna ya kikandamizaji kwani wale wanaoongoza wanawakandamiza wale wanaowaongoza. Hili limedhihirishwa katika *Lina Ubani*. Mwanahego anaeleza:

> *Kamwambie baba yako hayo maneno ya ugoro. Usituambie sisi kutugeuza bwege. Asiyefanya kazi wewe uliye juu ya kilima. Juu ya kilima kuna mashamba? Asiyefanya kazi baba yako anayekula vya bure, unavyomletea wewe* (Mlama, 1984: 45 - 46).

Mara nyingi, uhalisi huongezewa ubunifu ili kuifanya matini iwe na vionjo vya kifasihi. Vionjo hivyo ndivyo vinavyoifanya kazi inayohusika iitwe kazi ya kifasihi. Kwa kuwa maneno anayoongea Mwanahego yanaonekana ni ya mwendawazimu, basi ndani yake yanaonekana kuwa na vionjo vya kifasihi, ukiwamo ucheshi ambao ni sehemu ya vionjo hivyo. Ucheshi huo unafanya kazi iwe ya kuvuta makini ya watazamaji na wasomaji wa kazi hiyo. Ucheshi huchangamana na uhalisi wa kazi yenyewe ya kibunifu; na hivyo, kuifanya hadhira icheke wakati huo huo ikiwa inajifunza kutokana na ukweli ulioambatana na ucheshi (Muhanika, 1982). Ikitokea makosa au hitilafu havijatambuliwa au kufahamika vinaleta vichekesho. Hata hivyo, kutambua hitilafu sawasawa ni hali inayolazimisha ucheshi pia. Jambo hili linadhihirishwa na maneno ya Mwanahego yanayoonesha kuwapo kwa tofauti kubwa baina ya viongozi na wananchi wa kawaida.

### 1.3.5 Ukweli kuhusu mahitaji ya kila siku

Suala la mahitaji ya msingi ya binadamu linagusa maisha ya kila siku ya mwanajamii yeyote katika jamii inayohusika. Baadhi ya mahitaji muhimu ya kila siku kwa kila mtu ni malazi, mavazi na chakula. Mahitaji hayo ndiyo yanayomfanya mtu yeyote kujishughulisha ili aweze kujikimu kimaisha. Suala la mahitaji hutegemea sana suala la uchumi, lakini kuna tofauti ndogo kati ya mambo hayo mawili, hasa unapochunguza mahitaji ya wahusika. Mwandishi amejaribu kuonesha utofauti huo kwa kuwatumia wahusika wake wote. Kukosekana kwa mahitaji ya kila siku, kulimfanya mke wa Mwanahego kwenda kwao na watoto wake wote ili waweze kujikimu katika mahitaji ya chakula. Suala hili lilimfanya Mwanahego kubwatuka maneno mengi mbele ya viongozi, lakini alipuuzwa kwa kile alichokuwa anakisema.

Kuwepo kwa uhujumu uchumi uliokithiri katika jamii ulimfanya Mwanahego aseme tu bila kujali. Ujasiri wake wa kusema bila kuhofu lolote ulimfanya atazamwe kama mlevi tu. Jambo hilo linatokana na hali ya ubongo wa mlevi kuwa umeharibiwa na pombe (Culwell, 1994). Mlevi huwa anaongea tu bila kuwa na ufahamu wa kile anachokiongea; na haimfanyi kutambua kwamba amesema ukweli. Inafahamika wazi kwamba kilevi kinaondoa aibu ya kujizuia, lakini hakimfanyi mlevi kusema kweli katika mambo yote kwa kuelezea hisia ambazo kwa kawaida hazisemwi kwa sauti. Kilevi sio sababu ya kumfanya aseme kweli zaidi ya mtu aliye katika hali ya akili timamu, bali kinarahisisha tu namna ya kuelezea baadhi ya hisia, ambazo watu wote wanazo katika maisha ya kila siku. Hata hivyo, imekuwa tofauti na mhusika mwenyewe anavyoeleza yale yaliyo moyoni mwake. Mwandishi anamchora

kwa kusema kuwa hela za kigeni….unazitaka wewe unayekula vya kigeni. Mie nataka hela za hapa hapa…nipate nauli nikamchukue mke wangu… na mwanangu Kidote. Mchicha nanunua kwa shilingi tu… ukimpa ya Malkia anakataa… hela ya kigeni? Aka! (Nyoni, 2007: 27).

Maneno hayo ya mhusika mlevi yanaakisi hali halisi ya jamii ya Mwanahego na kuimulika huku ikionesha kuwa mahitaji ya kila siku ni ya shida. Pia, anaonesha kuwa viongozi wana matumizi ya fedha za kigeni, lakini watu wa kawaida hawajui hata hizo fedha za kigeni zina umuhimu gani na zinatumikaje hapa nchini (Mng'ong'o, 1980). Kukosa fedha ndiko kulikomfanya mke wa Mwanahego aende kwao na watoto wake wote. Maneno ya Mwanahego yanaleta ucheshi kwa kukejeli viongozi ambao wanang'ang'ania fedha za kigeni, lakini wananchi hawazijui hata zilivyo. Kejeli hiyo ndiyo inayoibua ucheshi unaoleta hamaki kwa hadhira. Watu wanaishi kwa shida ya chakula na kuhangaika bila mafanikio; viongozi wanataka watu waendelee kulima mazao ya biashara ili waipatie serikali fedha za kigeni. Ucheshi unaweza kutumika kama mbinu ya kumdhalilisha mtu, kundi au taasisi (Berkowitz, 1970). Ucheshi husababishwa na kushushwa hadhi kwa mtu kutokana na masuala ya kijamii au kimaumbile.

Kwa kawaida, ucheshi unajibainisha katika kile kinachoelezwa na msemaji wa kazi ya fasihi. Vilevile, hutokea baada ya kugundua ukweli uliopo katika kauli za mhusika mlevi. Mabepari nao wanaonekana kuwa na mikakati na mipango imara inayofanya kazi ya kuzuia watu kupata urazini wa kufanya mapinduzi ya kimkakati na kimaisha. Mkakati wa kuondoa maarifa ya mawazo ya tabaka tawaliwa ili wasiweze

kufikiria kujikomboa kiuchumi unafanywa na mataifa ya kibepari. Jambo hili linamfanya Mwanahego aingiwe na hofu na kuanza kuropoka tu yale yaliyo kweli. Wengine wanahofu kuwa Mwanahego atafungwa kutokana na maneno yake makali. Udhanifu wa kuwafanya watu wafikiri kujikomboa katika ngazi zote za kimaisha, umejazwa fikra za kuwaletea hofu wananchi kuusema ukweli.

## 2.0 Hitimisho na Mapendekezo

Makala haya yamechunguza muakiso wa ukweli wa kauli za mlevi kwa kurejelea tamthiliya za *Lina Ubani* na *Mabepari wa Bongo*. Uchunguzi umezingatia uhalisi wa kauli za mhusika mlevi kwa kurejelea vitabu vilivyobainishwa. Pia, makala yametalii jinsi matendo na kauli za mhusika mlevi zilivyoakisiwa katika fasihi ya Kiswahili. Kuakisiwa huko kumetazamwa kifasihi zaidi. Kimsingi, mhusika mlevi amejengwa kisanaa kama mbinu mojawapo ya ukwepaji wa changamoto mahsusi zinazotazamwa kwa jicho la kiuchunguzi, hasa anapoeleza wazi wazi masuala yanayoigusa jamii na serikali yake. Hali hiyo inaonesha kuwa mhusika mlevi ni msemaji wa mambo yanayomsibu mwandishi. Nafasi hiyo humpa mwandishi fursa pana ya kutamba na kutambaa kwa kadiri anavyoweza kuyaweka wazi mambo yote yanayoshindikana kusemwa na wahusika walio katika ung'amuzi tambuzi.

## Marejeleo

Arthurs, S. (1858). *Ten night in bar room*. New York.

Bakola, E. (2006). *Cratinus and the art of comedy*. New York: Oxford University Press.

Berkowitz, L. (1970). Aggressive humor as a stimulus to aggressive responses. *Journal of Personality and Social Psychology*, *16*, 710–717.

Chapman, A. J. (1976). *Humour and laughter theory: Research and applications*. London: Wiley and Sons limited.

Culwell, M. L. (1994). The role of the clown in Shakespeartheatre, katika *shaksper.net/scholarly-resources/library-of-essays.* Ilipakuliwa tarehe 13/08/2020.

Davidson, B. (1970). *The growth of African civilisation*. Nairobi: Longman.

Dickens, C. (1954). *Drunkard's deathkatika*http://www.daily-pulp.com/literature/the-drunkards-death. Ilipakuliwa tarehe 17/08/2020.

Faulkner, P. (1977). *Modernism: The critical idiom*. London: Methuen and Co Ltd.

Freud, S. (1896). Aetiology of neuroses, *katika* www.freudmuseum.at/freud/chronolg/1896-e.htm. Ilipakuliwa tarehe 12/08/2020.

Freud, S. (1923). The ego and the id. *Katik*a *Wikipedia*, *The Free Encyclopedia*. Tarehe 12/08/2020.

Freud, S. (1900). *The interpretation of dreams*. Katika http://en.wikipedia.org/wiki/Psychoanalysis #cite_note-12. Ilipakuliwa tarehe 22/05/2020.

Frosch, N. (1964). Psychoanalysis, katika *Wikipedia*, *The Free Encylopedia*.Ilipakuliwa tarehe 12/06/2020.

Godkewitsch, M. (1996). *Physiological and verbal indices of arousal in rated humour and laughter theory; Research and Applications*. London: Wiley and Sons limited.

Kedmon, P. (2010). Mlevi anapolewa chakari, *katika* Mtandao wa maisha na mafanikio. Ilipakuliwa tarehe 14/06/2020.

Kezilahabi, E. (1975). *Rosa Mistika*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E.  (2008). *Karibu ndani*. Dar es Salaam University Press.

Legulegu, S. (2016). *Siasa na uchumi katika fasihi ya Kiswahili*. Tasnifu ya Shahada ya Kwanza (Haijachapishwa). Arusha: Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

Makras, K (2010). Dickens interperance: The presentaion of drunkard in *The Drunkard's Death and The Pickwick* Papers.

Matteru, M. O. B (1982). *The image of the women in Tanzania oral literature: A survey* katika Kiswahili. Jarida la TUKI: Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Juzuu la 49, Toleo la 2.

Mayega, P. (2006). *Mwalimu mkuu wa watu*. Dar es Salaam: MBP Interprises.

Mbonde, J. P. (2002). Uchambuzi na uhakiki katika *Janga Sugu la Wazawa*. Swahili Forum 12 (2005): 81–93.

Mlacha, S. A. K. (1985). Wahusika katika riwaya za Kiswahili. Makala katikaMULIKA Na: 17. TUKI.

Muhando, P. (1984). *Lina ubani*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Muindi, A. (1996). *Usawiri wa wahusika makahaba katika vitabu vya Said Ahmed Mohamed*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mng'ong'o, C. G. (1980). *Njozi iliyopotea*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mnigo, R. A. (2015). *Tathmini ya mwingiliano matini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo: Utafiti linganishi wa tamthiliya yaNgoma ya Ng'wanamalundi* na *Fumo Liongo*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Moliere, G. (1911). *The doctor In spite of himself*.Dublin: Maunsel &Company Ltd.

Mohamed, S. M. (1995). *Amezidi*. Hardcover: East African Educational publishers.

Selden, R*et al*. (2005). *A reader's guide to contemporary literary theory*. New York: Longman.

Muhanika, H. (1982). Killer drink and other stories. Dar es Salaam: Publicity International Ltd.

Nyerere, J. K. (1974). *Binadamu na maendeleo*. Oxford: Oxford University Press.

Nyerere, J. K. (1968). *Ujamaa*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Nyoni, F. P. (2007). *Mabepari wa bongo*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

O'cannor, F. (1948). *The drunkard*. USA: New York.

Senkoro, F. E. M. K. (2004). Fools, drunkards and imbeciles tell more truth: Whither satire in Tanzania? *katika* (mh) Y. M. Kihore,*Kiswahili: TUKI, JUZUU Na. 67*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Selden, R., et al. (2005). *A reader's guide to contemporary literary theory*. New York: Longman.

Senkoro, F. E. M. K. (2006). Fasihi ya Kiswahili ya majaribio: Makutano ya fasihi simulizi na fasihi andishi.*Kioo cha Lugha, JUZUU Na 4*. Idara ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Shakespeare, W. (1990). *The taming of the shrew*. New York: Oxford University Press.

Shemweta, D. (2015). *Itikadi katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo: Utafiti linganishi wa Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liongo.* Tasnifu ya shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Shivji, I. (2002). *Makuadi wa soko huria* (Chachage, S. C) (mh), Hotuba ya Uzinduzi wa Kitabu. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI katika Mulika 26: 17–24.

Tutuola, A. (1993). *Palm wine drunkard*. Grove Press.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya fasihi 1: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa.

Wilder, T. (1930). *Our town*. New York: Harper Perennial.

William, J *at el*., (1976). Humour as a creative experience: The developmen of Hollywood humour, *katika*T. Chapman, T & F. Hugh. (wah), *Humour and laughter theory; Research and applications*. London: Wiley ana Sons limited.

Younge, R. (1638). *The drunkard's character* or *a true drunkard with such sinnes a raigne in him*. London: Folger Education.